

**Mfululizo wa Masuala ya Kifikihi**  
**al-Basmallah: Juz'iyatuhaa wa 'l-Jahrubihaa**

**BISMILLAH**

**Ni sehemu ya Qur'ani**  
**na**  
**Husomwa kwa Jahara**

**Kwa mujibu wa Kitabu na Sunna**

Kimeandikwa na:  
**Sheikh Ja'far Subhani**

Kimetafsiriwa na:  
**Hemedi Lubumba Selemani**

**Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**

**AL-ITRAH FOUNDATION**

**ISBN: 9987 - 427 - 44 - 8**

Kimeandikwa na:

**Sheikh Jafar Subhani**

Kimetafsiriwa na:

**Hemedi Lubumba Selemani**

Kimehaririwa na:

**Ustadh Abdallah Mohamed**

Kupangwa katika Kompyuta na:

**Ukhti Pili Rajab**

Toleo la kwanza: Machi, 2008

**Nakala: 1000**

Kimetolewa na kuchapishwa na:

Alitrah Foundation

P.O. Box 19701 Dar es Salaam, Tanzania

Simu:+255 22 2110640

Simu/Fax: +255 22 2127555

Email: alitrah@raha.com

Website: www.alitrah.org

Online: www.alitrah.info

# YALIYOMO

Bismillahi ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa kudhihirishwa.....	2
Ubora wa Bismillahi.....	6
Kauli za wanazuoni wa Fiq'hi kuhusu usehemu wa Bismillahi.....	7
Bismillahi ni sehemu ya surat Al-Fatihah.....	10
Sab- u'l-mathani (Saba zimwazo mara kwa mara ni surati Al-Fatihah.....	15
Al-hamdu, ufunguo wa kitabu ni Aya saba iwapoo pamoja na Bismillahi.....	21
Riwaya za Maimamu wa Ahlul Bayt.....	22
Bismillahi na ulazima wa kudhihirishwa.....	24
Maimamu wa Ahlul-Bayt na kudhihirisha Bismillahi .....	30
Hoja za mwenye kudai kuwa Bismillahi si sehemu ya Al-fatihah au haidhihirishwi.....	32
Zinazopingwa na historia sahihi.....	38
Bismillahi ni sehemu ya mwanzo wa kila sura.....	41

.

## NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu kilichoko mikononi mwako, ni tarjuma ya kitabu cha Kiarabu kwa jina la: **“al-Basmallah: Juz’iyyatuhaa wa ‘l-Jahrubihaa”** Sisi tumekiita: **“Bismillah ni sehemu ya Qur’ani na husomwa kwa Jahara.”**

“Kitabu hiki, **“Bismillahi ni sehemu ya Qur’ani na husomwa kwa Jahara.”** ni matokea ya utafiti wa kielimu uliofanywa na Mwanachuoni wa Kiislamu, **Sheikh Jafar Subhany.**

Sheria ya Kiislamu ni ya kipekee kwa kuwa inahusika na kila jambo huku ikiweka utatuzi wa matatizo yote yanayompata mwanadamu katika sekta zote za maisha yake.

Wanachouni wa Kiislamu kama kawaida ya wanadamu wamehitilafiana katika hukumu ndogo ndogo katika matendo ya ibada, lakini kama ilivyo, tofauti ndogo kati ya wanachuo kwa wafuasi inakuwa ni mlima wa tofauti na kusababisha zongo lisilo na maana. Mambo ambayo wanachuo wetu wamehitilafiana si katika asili au misingi ya dini, na isitoshe ni mambo machache sana ukilinganisha na yale tunayokubaliana nayo.



**BISMILLAH** ni Aya? Hili ni suala ambalo wanachuo wetu wamehitalifiana; ndani ya madhehebu moja na kati ya madhehebu. Kwa hiyo hii sio hitilafu ya madhehebu, bali ni hitilafi ya wanachuo wa madhehebu zote, wamehitilafiana juu ya suala hili. Lakini bahati mbaya Waislamu wengi hawaitambui hitilafu hii kwa usahihi na hivyo kuongelea katika dhana na kusababisha mizozo isiyokuwa na maana. Kutokana na hali hii Sheikh wetu, Jafar Subhani amelifanyia utafiti wa kina suala hili na kuweka wazi asaili ya hitilafu hii, kisha akamuachia msomaji mwenyewe kutoa uamuzi.

Kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote. Kutokana na ukweli huu, Taasisi

yetu ya 'Al-Itrah Foundation' imeona ikitoe kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili, kwa madhumuni yake yale yale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili, ili kuongeza ujuzi wao katika masuala ya dini na ya kijamii.

Tunamshukuru ndugu yetu, **Hemedi Lubumba Selemani** kwa kukubali jukumu hili la kukifanyia tarjuma kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwa kitabu hiki.

**Mchapishaji:**  
**Al -Itrah Foundation**  
**S. L. P. 19701**  
**Dar-es-Salaam, Tanzania.**





## Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara

### BISMILLAH NI SEHEMU YA QUR'ANI NA HUSOMWA KWA JAHARA, KWA MUJIBU WA KITABU NA SUNNAH

Kila sifa njema ni za Mwenyezi Mungu mlezi wa ulimwengu. Rehma na Amani zimfikie mbora wa viumbe na hitimisho la mitume wake, pia kizazi chake kitakatifu ambacho ndio kasha la elimu yake na hazina ya mafunzo yake.

Hakika Uislamu ni imani na sheria. Imani ni kuamini Mwenyezi Mungu, Mitume Wake na Siku ya Mwisho. Na sheria ni hukmu za Mwenyezi Mungu ambazo zina jukumu la kumpa mwanadamu maisha bora na kumhakikishia wema wa dunia na akhera.

Sheria ya Kiislamu ni ya kipekee kwa kuwa inahusika na kila jambo huku ikiweka utatuzi wa matatizo yote yanayompata mwanadamu katika sekta zote za maisha yake, hivyo Mwenyezi Mungu akasema:

الْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتَمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ  
الْإِسْلَامَ دِينًا

**“Leo nimewakamilishieni dini yenu na kuwatimizieni neema yangu na nimewapendeleeni Uislamu uwe dini yenu ( 5:3 ).**

Isipokuwa kuna masuala madogomadogo ambayo wanazuoni wa sheria wametofautiana kwa sababu ya kutofautiana kwao kuhusu riwaya ambazo zimenasibishwa kwa Mtume. Jambo ambalo limepelekea kutofautiana kuhusu masuala madogo madogo ya sheria.



## Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara

Kwa kuwa ukweli hutokana na utafiti basi hakika katika mtiririko wa masomo haya tumejaribu kuliweka swala hili juu ya meza ya utafiti, kwani huenda ikawa ndio njia ya kuunganisha mitazamo na kupiga hatua katika uwanja huu. Kwani tofauti iliyopo si katika asili na misingi ya dini hata ipelekee kuwa na uadui na chuki bali tofauti iliyopo ni kuhusu riwaya zilizozanasibishwa na Mtume, nalo ni jambo dogo ukilinganisha na mambo mengi ambayo tunaafikiana kati ya madhehebu za Kiisilamu. Na muongozo wetu katika njia hii ni kauli ya Mwenyezi Mungu:

وَأَعْتَصِمُوا بِحَبْلِ اللَّهِ جَمِيعًا وَلَا تَفَرَّقُوا ۗ وَاذْكُرُوا نِعْمَتَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ  
كُنْتُمْ أَعْدَاءً فَأَلَّفَ بَيْنَ قُلُوبِكُمْ فَأَصْبَحْتُمْ بِنِعْمَتِهِ إِخْوَانًا ﴿١٣﴾

"Na shikamaneni na kamba ya Mwenyezi Mungu nyote wala msifarakiane. Na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yenu, mlipokuwa maadui na akaziunganisha nyoyo zenu, hivyo kwa neema zake mkawa ndugu." (3:10 3).

Sheikh Jafar Subhany  
Tasisi ya Imamu Sadiq (a.s.)  
Qum

## Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara

### Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara

Kilugha na kiistilahi neno *Basmala* hutumika kumaanisha tamko: *Bismillahi Rahmani Rahimu*.

Husemwa ndani ya Kiarabu: *Basmala basmalatan*. Humaanisha ameandika au ametamka: *Bismillahi*.

Husemwa ndani ya Kiarabu: Amekithirisha *Basmala*. Yaani amezidisha kusema: *Bismillahi*.<sup>1</sup>

Bismillahi ndio alama ya Waislamu kiasi kwamba hawaanzi kitu isipokuwa baada ya kutaja *Bismillahi Rahmani Rahim*. Nayo ni Aya ya Tawhidi na sababu ya kuchukua washirikina.

Mwenyezi Mungu amesema: **“Na wanapoambiwa: Msujudieni Rahmani, husema: Ni nani Rahmani? Je, umsujudie unayetuumuru? Na inawazidishia chuki.”**<sup>2</sup>

Mbiu ya washirikina zama za ujahiliya ilikuwa ni kauli: *Bismika llahuma* (Kwa jina lako wewe Mwenyezi Mungu). Walikuwa wakianza maneno yao kwa tamko hilo.

Katika suluhu ya Hidaybiyya ililazimika kuandika mkataba wa suluhu kati ya pande mbili, Mtume akamuamrisha Ali (a.s.) aandike: *Bismillahi Rahmani Rahim*. Akaandika kama alivyoamrisha. Hapo Suhaylu mwakilishi wa Maqurayshi akasema: “Silijui hili, bali andika: *Bismika llahuma*. (Kwa jina lako ewe Mwenyezi Mungu).<sup>3</sup>

1. *Lisanul-Arabu wal-misbahu al-muniru*: Neno *Basmalatu*.

2. *Al-Fur'qani*: 60

3. *Siratu Ibnu Hishamu*: 2 / 317

## **Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara**

Hivyo Bismillahi ndio mpaka unaotenga kati ya Uislamu na shirki, na kwa hiyo Bismillahi hutofautisha kati ya muumini na kafiri, na wala Muislamu haachani na Bismillahi popote pale alipo.

Bismillahi ni Aya ya Qur'ani kwa ushahidi wa misahafu karne zote nenda rudi. Na Bismillahi imeandikwa mwanzo wa kila Sura ya Qur'ani isipokuwa Suratut-Tauba.

Wameiandika Bismillahi kama walivyoandika Aya nyingine bila tofauti yoyote huku wakikubaliana kuwa wasiandike kitu chochote kile kisicho Qur'ani ndani ya Qur'ani isipokuwa ni lazima wakiwekee kitu hicho alama tenganishi inayotofautisha ili kitu chochote kisicho Qur'ani kisi-jichanganye na Qur'ani.

Kwa ajili hiyo ndio maana utawaona wametofautisha Qur'ani na majina ya Sura zake, idadi ya Aya zake, alama za juzuu zake, robo zake, rukuu zake na sijda zake. Hayo yote wameyaandika kwa namna ambayo yanatengana na Qur'ani na kuwa nje ya Qur'ani.

Wakati huo huo tangu mwanzo mpaka leo wamekubaliana kuandika Bismillahi mwanzo wa kila Sura kama wanavyoandika Aya nyingine bila alama yoyote tenganishi.

Wala hutoikuta Qur'ani iliyoandikwa toka enzi za maswahaba mpaka leo isipokuwa itakuwa katika namna hiyo. Na hili ni makubaliano ya kiviten-do toka kwao kuwa Bismillahi ni sehemu ya msahafu.

Isipokuwa baada ya kufariki Mtume kulitokea tofauti, na dhahiri ni kuwa tofauti hii ilitokea wakati wa utawala wa Mu'awiyah bin Abi Sufiani au kabla yake kidogo.

## **Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara**

Ama chanzo cha kuzuka tofauti husika, huenda baadhi ya sababu ni kutaka kukhalifu mwenendo wa Imam Ali (a.s.) katika Bismillahi, kwani watu wote wamekubali kuwa Ali bin Abi Talib alikuwa akidhihirisha Bismillahi.

Razi amesema: "Ama Ali bin Abi Talib yeye alikuwa akidhihirisha Bismillahi na hilo limethibiti kwa wingi. Alikuwa akisema: "Ewe ambaye utajo wake ni sharafu kwa wenye kumtaja." <sup>4</sup>

Na kuna riwaya nyingi toka kwa Mtume na kizazi chake zinazothibitisha kuwa Bismillahi ni sehemu ya Surat Al-Fatihah, na kuwa ni lazima kuisoma kwa kudhihirisha sauti katika Swala za kudhihirisha na kuwa yenyewe ni sehemu ya kila Sura.

Ukweli huu utadhihirika katika vifungu vifuatavyo:

## **Ubora wa Bismillahi**

Kuna hadithi nyingi zimepokewa kuhusu ubora wa Bismillahi, nasi hapa tutachukua chache tu:

Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: "Nimefanywa bora kwa *Bismillahi Rahmani Rahim.*" Na akasema: "Haijamshukia yeyote asiyekuwa mimi isipokuwa ile alioielezea Mwenyezi Mungu Mtukufu katika barua ya Selemani."<sup>5</sup>

Imamu Al-Baqir (a.s.) amesema: "Aya bora mno ndani ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu ni: Bismillahi Rahmani Rahim."<sup>6</sup>

Sheikh Tusi ametoa toka kwa Abdallah bin Yahya Al-Kahiliy toka kwa

---

4. *At-Tafsirul-Kabir*: 1/204

5. *Kanzul-ummali*:1/655 namba 2492. *Tafsiri Ibnu Kathiri*:1/17. *Biharul-Anuwar*: 89/227 namba 4

6. *Tafsirul-Iyashi*: 1/19 namba 4

## **Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara**

Sadiq (a.s.) toka kwa baba yake amesema: “Bismillahi Rahmani Rahim ndio iliyo karibu mno na jina tukufu la Mwenyezi Mungu kuliko ukaribu wa mboni ya jicho kwenye weupe wake.”<sup>7</sup>

## **Kauli za wanazuoni wa Fiq'hi kuhusu usehemu wa Bismillahi**

Al-Qurtubiy ametaja kauli za Maimam wanne kwa uwazi akasema: “Wametofautiana kuhusu kusoma Bismillahi Rahmani Rahim mwanzo wa kisomo ndani ya Swala.”

1. Malik kakataza kufanya hivyo ndani ya Swala ya faradhi - iwe kwa kimya au kwa kudhihirisha - sawa iwe mwanzo wa kuanza Al-Hamdu au Sura nyingine, na ameruhusu hilo katika Swala za Sunna.

2. Abi Hanifa na Athauriyu na Ahmad wamesema: “Aisome pamoja na Al-Hamdu kwa kimya ndani ya kila rakaa.”

3. Shafi'i amesema: “Aisome, na ni lazima aidhihirishe katika Swala za kudhihirisha na aisome kwa moyo katika Swala za kuficha. Na kwa Shafi'i yenyewe ni Aya katika Surat Al-Fatihah. Na kauli hii ya kuwa ni Aya katika Surat Al-Fatihah ndio kauli ya Ahmad, Abi Thauru na Ubaydu.

Imetofautiana kauli ya Shafi'i kuhusu je, yenyewe ni Aya ndani ya kila Sura au ni Aya ndani ya Surat Namlu tu na Surat Al-Fatihah? Kwani katika hilo zimepokewa kauli zote mbili kutoka kwake.

Sababu ya kutofautiana kuhusu suala hili ni mambo mawili:

La kwanza: Ni kutofautiana riwaya katika mlango huu.

La pili: Ni kutofautiana kwao kuhusu je, Bismillahi Rahmani Rahim ni Aya

---

7. At-Tahdhibu: 2/289, namba 1159

## Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara

ndani ya Surat Al-Fatihah? Au si Aya.<sup>8</sup>

Shekh Tusi amesema: “Bismillahi Rahmani Rahim ni Aya ndani ya kila Sura ndani ya Qur'ani yote, nayo ni Aya ya mwanzo ndani ya Surat Al-Hamdu.”

Shafi'i amesema: “Hakika yenyewe ni Aya ndani ya Surat Al-Hamdu bila tofauti yoyote kati yao.” Ama kuhusu kuwa yenyewe ni Aya ndani ya kila Sura, kuna kauli mbili:

Mojawapo ni : Yenyewe ni Aya mwanzo wa kila Sura. Na nyingine ni: Yenyewe ni sehemu ya Aya ndani ya kila Sura. Hivyo hutimia na kuwa Aya kamili pale inapokuwa pamoja na sehemu inayofatia baada yake.

Ahmad, Is'haqa, Abi Thauri, Abi Ubayda, Atau, Az-Zahriyu na Abdallah bin Mubarak wamesema: Hakika yenyewe ni Aya mwanzo wa kila Sura, mpaka Abdallah bin Mubarak akasema: “Atakayeacha Bismillahi Rahmani Rahim atakuwa kaacha Aya mia moja na kumi na tatu.”

Abi Hanifa, Malik, Al-Awzaiyu na Daudi wamesema: “Yenyewe si Aya ndani ya Surat Al-Fatihah wala ndani ya Sura nyingine.”

Malik, Al-Awzaiyu, na Daud wamesema: “Ni karaha kuisoma ndani ya Swala bali atowe tak'bira na aanze Al-Hamdu isipokuwa ndani ya mwezi wa Ramadhani, na Sunna ni kuisoma kati ya Sura mbili ili kuzitenganisha, na wala asiisome mwanzo wa Surat Al-Fatihah<sup>9</sup>.”

Matokeo ya kauli hizi ni kuwa: Malik haoni kuwa Bismillahi ni sehemu ya Sura yoyote. Ama wafuasi wa Hanafi na Hambali wanaona kuwa ni sehemu ya Surat Al-Fatihah lakini wanaisoma kwa siri.

Ama wafuasi wa Shafi'i wanaona ni sehemu ya Surat Al-Fatihah, na wanaisoma kwa kudhihirisha katika Swala za kudhihirisha na kwa kuficha katika Swala za kunong'ona (Adhuhuri na Alasiri). Ama je, yenyewe ni sehe-

8. *Bidayatul-Muj'tahid*: 1/124

9. *Al-Khilafu*: 1/327, mas'ala ya 82 kitabu cha sala.

## Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara

mu ya Sura nyingine, hapo kwa Shafi'i kuna kauli mbili.

Ama Shia Imamiyya wao hawana isipokuwa kauli moja tu, nayo ni kuwa Bismillahi ni sehemu ya kila Sura, na ni wajibu kuidhihirisha ndani ya Swala za kudhihirisha, na ni Sunna kuidhihirisha ndani ya Swala za kunong'ona.

Na kauli iliyo mbali sana na Shia Imamiyya ni kauli ya Malik, kwani Bismillahi kwake si Aya ndani ya Qur'ani isipokuwa ile ya Surat Namlu yenyewe ni sehemu ya Aya, na ni karaha kwa Imam na asiye Imam kuso- ma Bismillahi ndani ya Swala ya faradhi kabla ya Al-Fatihah au kusoma Sura baada yake.

Ina nafasi gani kauli hii mbele ya maneno ya Imam As-Sadiq (a.s.) ambaye amesema akimlaumu yule anaeacha Bismillahi ndani ya Swala na kuona kuwa kuidhihirisha ni bidaa, hivyo akasema: "Wana nini, wameizushia uongo makusudi Aya tukufu mno ndani ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu wakadai eti ni bidaa wanapoidhihirisha, nayo ni Bismillahi Rahmani Rahim."<sup>10</sup>

Na ili kuhakiki mada hii inalazimu kutafiti mambo yafuatayo:

**Kwanza:** Je, Bismillahi ni sehemu ya Surat Al-Fatihah au hapana?

**Pili:** Tukijalia kuwa ni sehemu ya Surat Al-Fatihah, Je, inadhihirishwa ndani ya Swala za kudhihirisha au hapana?

**Tatu:** Je, Bismillahi ni sehemu ya Sura ndani ya Sura nyingine au hapana?

Na kwa idhini ya Mwenyezi Mungu tutatoa dalili za kauli husika pamoja na hukumu yenye kumaliza tatizo.

---

10. *Tafsirul-Iyashi*: 1/21, Hadithi 16

## Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara

---

# Bismillahi ni sehemu ya Surat Al-Fatihah

Hakika Bismillahi ni sehemu ya Surat Al-Fatihah, na dalili juu ya hilo ni mambo yafuatayo tutakayoyataja moja baada ya jingine.

**Kwanza:** Riwaya aliyoipokea Shafi'i kwa njia yake kuwa Muawiya alikwenda Madina akaswali hapo Madina, na wala hakusoma Bismillahi Rahmani Rahim, na wala hakutoa Takbira wakati wa kwenda rukuu wala wakati wa kwenda sijida. Alipotoa Salaam, Muhajirina na Answare wakasema: "Ewe Muawiya, umeiibia Swala, iko wapi Bismillahi Rahmani Rahim?! na iko wapi takbira wakati wa kurukuu na kusujudu?!" Kisha akawa amerudia Swala ikiwa na Bismillahi na takbira.

Shafi'i amesema: "Hakika Muawiya alikuwa mtawala mwenye nguvu kubwa, mwenye makali, hivyo laiti kama kudhihirisha Bismillahi kusingekuwa ni jambo lililokubalika kwa maswahaba wote Muhajirina na Answare basi wasingeweza kudhihirisha ukosoaji wao kwake kwa sababu ya kuacha Bismillahi."<sup>11</sup>

Na sisi tunasema: Na laiti Bismillahi isingekuwa ni sehemu ya Al-Fatihah basi Muhajirina na Answare wasingemkosoa kwa kuiacha, huku akiwa kaacha tu kuidhihirisha.

Riwaya hii kama inavyohibitisha kuwa Bismillahi ni sehemu ya Al-Hamdu inathibitisha pia ulazima wa kuidhihirisha, hivyo tunaitumia kama dalili sehemu nzote mbili.

---

11. *Musnad Shaafiyyu: 13.* Razi ameinukuu kwa ukamilifu ndani ya tafsiri yake *Al-Kabir: 1/204* na *Al-Mustadrak: 1/233*



## **Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara**

**Pili:** Shafi'i amepokea toka kwa Muslim toka kwa Ibnu Jariji toka kwa Ibnu Abi Malikatu toka kwa Ummu Salama kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu alisoma Al-Fatihah akaahesabu Bismillahi Rahmani Rahim kuwa ni Aya\*

(Kila sifa njema ni za Mwenyezi Mungu, Mola wa viume) ni Aya\*

(Mwingi wa rehema mwenye kurehemu) ni Aya\*

(Mwenye kumiliki siku ya malipo) ni Aya\*

(Wewe tu tunakuabudu, na kwako tu tunataka msaada) ni Aya\*

(Tuongoze njia iliyonyooka)\*

(Njia ya wale uliowaneemesha, siyo ya waliokasirikiwa, wala ya waliopotea)<sup>12</sup>

Maelezo haya yako wazi kuwa yenyewe ni sehemu ya Al-Hamdu.

Tatu: Al-Hakim ametoa toka kwa Ummu Salama kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu alisoma ndani ya Swala:

(Bismillahi Rahmani Rahim ) na akaihesabu kuwa ni Aya moja.

(Kila sifa njema ni za Mwenyezi Mungu, Mola wa viume) ni Aya mbili\*

(Mwingi wa rehema, mwenye kurehemu) ni Aya tatu\*

(Mwenye kumiliki siku ya malipo) ni Aya nne\*

---

12. *Al-Mustadrak*: 1/232

### **Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara**

Akasema: hivyo hivyo (Wewe tu tunakuabudu, na kwako tu tunataka msaada)\* akawa amekusanya vidole vyake vitano.<sup>13</sup>

**Nne:** Al-Hakim ametoa toka kwa Ummu Salama kuwa alisema: “Mtume alikuwa akisoma: Bismillahi Rahmani Rahim,\*

(Kila sifa njema ni za Mwenyezi Mungu, Mola wa viume) akiisoma herufi moja moja.

Al-Hakim amesema: “Hadithi hii ni sahihi kwa mujibu wa sharti za mashekhe wawili (Bukhari na Muslim) na hawajaitoa.

Na Adh-Dhahabiy ndani ya kitabu chake *Atal-khisi* amekiri usahihi wa hadithi hii<sup>14</sup>.

**Tano:** Al-Hakim ametoa toka kwa Naimul-Mujmiru amesema: “Nilikuwa nyuma ya Abi Huraira, akasoma Bismillahi Rahmani Rahim, akasoma Al-Hamdu mpaka akafika *Waladdhalina*, akasema: Amin. Watu wakasema: Amin. Na alikuwa kila anaposujudu husema: Allahu Akbar. Na anapotoa Salaam husema: “Naapa kwa yule ambaye nafsi yangu iko mikononi mwake hakika Swala yangu mimi ndio inayoshabihiana sana na Swala ya Mtume kuliko ninyi.”

Al-Hakim amesema: Hadith hii ni sahihi kwa sharti za mashekhe wawili na hawajaitoa, na ameipitisha Adh-Dhahabiy ndani ya *Talkhisi* yake.<sup>15</sup>

**Sita:** Al-Hakim ametoa toka kwa Qatada amesema: Anas bin Malik alilizwa: Kisomo cha Mtume wa Mwenyezi Mungu kilikuwaje? Akasema: “Ilikuwa ni kukokoteza, kisha akasoma: Bismillahi Rahmani Rahim.”<sup>16</sup> Ad-Dhahabi ameithibitisha ndani ya *Talkhisi* yake.

13. *Al-Mustadrak*: 1/232

14. *Al-Mustadrak*: 1/232

15. *Al-Mustadrak*: 1/232

16. *Al-Mustadrak*: 2/233

## Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara

**Saba:** Al-Hakim ametoa toka kwa Ibnu Jariji toka kwa baba yake toka kwa Said bin Jubairi toka kwa Ibnu Abbas kuhusu kauli ya Mwenyezi Mungu: (Na kwa hakika tumekupa Aya saba zisomwazo mara kwa mara na Qur'ani tukufu).

Akasema ni Al-Fatihah: Bismillahi Rahmani Rahim\* Kila sifa njema ni za Mwenyezi Mungu, Mola wa viumbe, akasoma Sura hiyo.

Ibnu Jariji akasema, nikamwambia baba yangu, je Sa'id amekuhabarisha kutoka kwa Ibnu Abbas kuwa Ibnu Abbas alisema: Bismillahi Rahmani Rahim ni Aya? Akasema: "Ndio."

Al-Hakim amesema: Hadithi hii ni sahihi na wala mashekhe wawili hawajaitoa, na mlango wote huu ndani ya kitabu cha Swala.<sup>17</sup>

**Nane:** Ath-Tha'labiyy ametoa kwa kupitia njia ya Abi Huraira amesema: "Nilikuwa na Mtume msikitini akaingia mtu na kuanza kuswali, akaanza Swala na kusoma *Audhubillahi* kisha akasema:

\* Kila sifa njema ni za Mwenyezi Mungu, Mola wa viumbe\* .

Mtume akamsikia akasema: "Ewe ndugu umejiharibia Swala yako, hivi hujui kuwa "Bismillahi Rahmani Rahim" ni sehemu ya Al-Hamdu? Atakayeacha basi ameacha Aya, na atakayeacha Aya basi amejiharibia Swala yake."<sup>18</sup>

**Tisa:** Ath-Tha'labiyy ametoa toka kwa Ali (a.s.) kuwa alikuwa aanzapo Sura ndani ya Swala husoma: "Bismillahi Rahmani Rahim", na alikuwa akisema: "Atakayeacha kuisoma basi amepunguza." Na alikuwa akisema: "Yenyewe ndio hutimiza saba zisomwazo mara kwa mara."<sup>19</sup>

17. *Al-Mustadrak*: 1/551, Tafsiri ya Surat Al-Fatihah.

18. *Ad-Durul-Manthur*: 1/21

19. *Kanzul-Ummal*: 2/297 namba 4049

## Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara

**Kumi:** Ath-Thalabiyy ametoa toka kwa Talha bin Abdallah amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: 'Atakaeacha "*Bismillahi Rahmani Rahim*" ameacha Aya toka ndani ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu, na katika yaliyohesabiwa kuwa ni mama wa kitabu katika yaliyoniteremkia mimi ni "*Bismillahi Rahmani Rahim*"<sup>20</sup>.

**Kumi Na Moja:** Ad-Darqutuniy na Al-Bayhaqiy ndani ya Sunan wametoa toka kwa Abi Huraira amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: Mtakapoisoma Al-Hamdu basi someni "*Bismillahi Rahmani Rahim*" haki-ka yenyewe ni mama wa Qur'ani na mama wa Kitabu na ni saba zisomwazo mara kwa mara ( Sabu'l-mathani) na Bismillahi Rahmani Rahim ni moja ya Aya zake."<sup>21</sup>

**Kumi na mbili:** At-Tabraniy ndani ya Al-Awsatu na Ad-Darqutuniy na Al-Bayhaqiy wote wameitoa toka kwa Nafi'u kuwa Ibnu Omar alikuwa aanzapo Swala huanza kwa kusoma "*Bismillahi Rahmani Rahim*" ndani ya mama wa Kitabu (Al-Hamdu) na katika Sura inayofatia, na anasema kuwa alisikia hilo toka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu."<sup>22</sup>

**Kumi na tatu:** Abi Daud na At-Tirmidhiy na Ad-Darqutuniy na Al-Bayhaqiy wametoa toka kwa Ibnu Abbas kuwa alisema: "Mtume alikuwa akianza Swala yake kwa "*Bismillahi Rahmani Rahim*."<sup>23</sup>

**Kumi na nne:** Ad-Darqutuniy na Al-Bayhaqiy wametoa toka kwa Abi Huraira kuwa Mtume alikuwa asomapo - ilhali akiwasalisha watu - huanza Swala kwa kusoma "*Bismillahi Rahmani Rahim*."

<sup>20</sup>. *Kanzul-Ummal*: 1/556 namba 2494

<sup>21</sup>. *Ad-Durul-mathur*: 1/11. *As-Sunnanil-Kubra*: 2/45

<sup>22</sup>. *Al-Mu'ujam al-Awsat*: 1/257. *As-Sunnanil-Kubra*: 2/48.

*Maj'maul-Zawaid*: 2/109

<sup>23</sup>. *At-Tirmidhiy*: 1/155 hadithi ya 245. *Sunanud-Darqutniy*: 1/303. *As-Sunnanil-Kubra*: 2/47

### **Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara**

Abi Huraira akasema: “Yenyewe ni Aya toka kwenye Kitabu cha Mwenyezi Mungu, isomeni mtakapo kusoma ufunguo wa Qur'ani hakika yenyewe ni Aya ya saba.”<sup>24</sup>

**Kumi na tano:** Al-Bayhaqiy ametoa ndani ya *Shaabul-Imani* toka kwa Ibnu Umar kuwa ndani ya Swala alikuwa akisoma “Bismillahi Rahmani Rahim” anapohitimisha Sura huisoma na husema: “Haikuandikwa isipokuwa ni kwa ajili ya kusomwa.”<sup>25</sup>

## **SAB-U’L-MATHANI (SABA ZISOMWAZO MARA KWA**

### **MARA NI SURATI AL-FATIHAH)**

Kuna riwaya nyingi zimepokewa toka kwa Ali (a.s.) na Ibnu Mas'udi na wengine miongoni mwa maswahaba na waliokuja baada ya maswahaba kuwa makusudio ya saba zisomwazo mara kwa mara ndani ya kauli ya Mwenyezi Mungu: “Na kwa hakika tumekupa saba zisomwazo mara kwa mara na Qur'ani tukufu.”<sup>26</sup> ni Surati Al-Fatihah. Huu ni upande mmoja.

Upande mwingine ni kuwa Aya za Surat Al-Fatihah hazifiki saba isipokuwa pale itakajumuishwa Bismillahi kuwa ni miongoni mwa Aya zake. Hivyo yafuatayo ni maelezo kuhusu pande hizo mbili:

Ama riwaya zinazoonyesha kuwa makusudio ya saba zisomwazo mara kwa mara ni Surati Al-Fatihah zipo katika makundi mawili:

24. *As-Sunanil-Kubra*: 2/47. *Sunanid-Darqutniy*: 1/305

25. *Shaabul-Imani*: 2/439-440, hadithi ya 2336

26. Al-Hij'ri: 87

## **Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara**

Zipo zinazotafsiri kuwa makusudio ya saba zisomwazo mara kwa mara ni Al-Hamdu bila kutamka wazi kuwa Bismillahi ni sehemu ya Al-Hamdu.

Na zipo zinazotafsiri kuwa makusudio ya saba zisomwazo mara kwa mara ni Al-Hamdu huku zikitamka wazi kuwa Bismillahi ni sehemu ya Aya zake.

Zifuatazo ni baadhi tu ya riwaya toka kundi la kwanza, na wala si zote kwa sababu kufanya hivyo kunawajibisha kurefusha wa maneno:

1. At-Tabari ametoa toka kwa Abdu Khayri toka kwa Ali (a.s.) kuwa amesema: “Saba zisomwazo mara kwa mara ni ufunguo wa Kitabu (Al-Hamdu).”<sup>27</sup>
2. At-Tabari ametoa toka kwa Ibnu Sirini amesema: Ibnu Mas'ud aliulizwa kuhusu saba zisomwazo mara kwa mara akasema: “Ni ufunguo wa Kitabu (Al-Hamdu).”<sup>28</sup>
3. At-Tabari ametoa toka kwa Al-Hasani kuhusu kauli ya Mwenyezi Mungu: “**Na kwa hakika tumekupa saba zisomwazo mara kwa mara.**” akasema: “Zenyewe ni ufunguo wa Kitabu (Al-Hamdu).” Na pia ametoa toka kwa Said bin Jubairi toka kwa Ibnu Abbas amesema: “Ni ufunguo wa Kitabu (Al-Hamdu).”
4. At-Tabari ametoa toka kwa Abi Fakhita katika Aya hii: “Na hakika tumekupa saba zisomwazo mara kwa mara, na Qur'ani tukufu.” amesema: “Ni mama wa Kitabu (Al-Hamdu).”<sup>29</sup>
5. At-Tabari ametoa toka kwa Abi Aliyatu katika kauli ya Mwenyezi Mungu: “**Na hakika tumekupa saba zisomwazo mara kwa mara.**”

---

27. *Tafsiri Tabariy*: 14/37

28. *Tafsiri Tabariy*: 14/37

29. *Tafsiri Tabariy*: 14/38

### **Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara**

amesema: “Ufunguo wa Kitabu ni saba zisomwazo mara kwa mara.”  
Nikamwambia Rabi'u, wao wanasema ni Sura saba ndefu. Akasema:  
“Iliteremka hii kabla hakijateremka chochote toka Sura ndefu.”

6. At-Tabari ametoa toka kwa Abil Aliyah amesema: “Ni ufunguo wa Kitabu. Akasema: Hakika imeitwa ni saba zisomwazo mara kwa mara kwa sababu mara kwa mara kila mtu asomapo Qur'ani huisoma. Akaambiwa Abi Aliyah: ‘Hakika Dhahaku bin Muzahimu anasema kuwa: Saba zisomwazo mara kwa mara ni Sura saba ndefu.’ Akasema: ‘Hakika Sura hii ya saba zisomwazo mara kwa mara ilishuka kabla hakijashuka chochote toka Sura ndefu.’”

7. At-Tabari ametoa toka kwa Abdallah bin Ubaydi bin Umayri amesema: “Saba zisomwazo mara kwa mara ni ufunguo wa Kitabu ( Al-Hamdu).”

8. At-Tabari ametoa toka kwa Ibnu Jariri toka kwa Ibnu Malikatu amesema: “Na hakika tumekupa saba zisomwazo mara kwa mara.” amesema: ‘Ni ufunguo wa Kitabu (Al-Hamdu). Na ufunguo wa Kitabu umetajwa kwa ajili ya Nabii wenu na wala hajatajiwa Nabii mwingine yoyote kabla yake.”

9. At-Tabari ametoa toka kwa Abi Huraira toka kwa Ubayya amesema: “Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: ‘Je, nikufundishe Sura ambayo haikuteremshwa ndani ya Tawrati wala ndani ya Injili wala Zaburi wala mfano wake ndani ya Qur'ani.’ Nikasema, ndio. Akasema: ‘Mimi natarajia kuwa hautotoka kwenye mlango ule isipokuwa utakuwa umejifunza.’ Hapo Mtume akasimama na nikasimama naye, akaanza kunihadithia ilihali mkono wake ukiwa ndani ya mkono wangu, nikaanza kutegea nikichukia asije akatoka kabla hajaniambia kuhusu Sura hiyo.

Alipokaribia mlangoni nikamwambia: ‘Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, Sura uliyoniahidi.’ Akasema: ‘Unasoma nini unapoanza Swala?’ Amesema: Akasoma Al-Hamdu. Mtume akasema: ‘Ndio yenyewe hiyo

### **Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara**

hiyo, nayo ndio saba ambayo husomwa mara kwa mara ambayo Mwenyezi Mungu amesema: **“Na hakika tumekupa saba zisomwazo mara kwa mara na Qur'ani tukufu”** ambayo nimepewa.”<sup>30</sup>

Hadithi hii kaitoa Al-Hakim ndani ya Al-Mustadrak na akasema ni hadithi sahihi kwa sharti za mashekhe wawili na hawajaitoa.<sup>31</sup>

10. At-Tabari ametoa toka kwa Abi Huraira toka kwa Mtume amesema: **“(Al-Hamdu) Yenyewe ni Mama wa Kitabu na ndio ufunguo wa Kitabu na saba zisomwazo mara kwa mara.”**<sup>32</sup>

11. At-Tabari ametoa toka kwa Abi Huraira toka kwa Mtume kuhusu ufunguo wa Kitabu (Al-Hamdu) amesema: Yenyewe ndio ufunguo wa Kitabu na saba zisomwazo mara kwa mara na Qur'ani tukufu.<sup>33</sup>

Ama zifuatazo ni riwaya za kundi la pili ambalo linatafsiri kuwa saba zisomwazo mara kwa mara ni Surat Al-Fatihah na kuweka Bismillahi kuwa ni Aya ya mwanzo katika Surat Al-Fatihah.

Ibnu Jarir na Abi Mun-dhiru na Tabaraniy na Ibnu Mar-dawihhi na Al-Hakim na Al-Bayhaqi ndani ya *Sunnani* yake wote wametoa toka kwa Ibnu Abbas kuwa aliulizwa kuhusu saba zisomwazo mara kwa mara. Akasema: ‘Ni ufunguo wa Kitabu (Al-Hamdu) ameiteua hasa kwa ajili ya umma wa Muhammad akaiinua kwa kuifanya ni Mama wa Kitabu akawahifadhia mpaka alipokuja kuwatolea na wala hakuna yeyote aliyepewa kabla yake. Akaambiwa: ‘Iko wapi Aya ya saba?’ Akasema: “Bismillahi Rahmani Rahim.”<sup>34</sup>

---

30. *Tafsir Tabari*: 14/40

31. *Al-Mustadrak*: 2/258

32. *Tafsiri Tabariy*: 14/41

33. *Tafsiri Tabariy*: 14/41

34. *Ad-Durul-Manthur*: 5/94



### **Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara**

At-Tabari ametoa toka kwa Said bin Jubairi katika kauli: “**Na hakika tumekupa saba zisomwazo mara kwa mara**” amesema: Ni ufunguo wa Kitabu (Al-Hamdu) Akaisoma kwa Aya sita kisha akesema: “Bismillahi Rahmani Rahim” ndio Aya ya saba. Said akasema: Ibnu Abbas alinisomea kama alivyokusomea, kisha akasema: Aya ya saba ni “Bismillahi Rahmani Rahim.”<sup>35</sup>

At-Tabari ametoa toka kwa Said bin Jubairi amesema: Ibnu Abbas aliniambia: Fungua, kisha akasoma ufunguo wa Kitabu (Al-Hamdu) kisha akasema: ‘Unajua kuwa ndio hii “**Na hakika tumekupa saba zisomwazo mara kwa mara.**”

Wala sentensi: “Fungua, kisha akasoma ufunguo wa Kitabu” haionyeshi kuwa Bismillahi haimo, kwa sababu kwa kuwa Bismillahi ipo mwanzoni mwa kila Sura ndio maana kaiashiria kwa kusema: “Fungua.” Kisha akaashiria Aya zake zinazotofautiana na Aya za Sura nyingine kwa kusema: Kisha akasoma ufunguo wa Kitabu (Al-Hamdu).

Na hadithi ifuatayo nayo inatafsiriwa kwa namna hiyo.

At-Tabari ametoa toka kwa Abi Said bin Amaaliy kuwa Mtume alimwita ilihali yeye akiwa ndani ya Swala, kwanza akaswali kisha ndio akaenda kwa Mtume. Mtume akasema: ‘Kitu gani kilikuzuwia usiitokie wito wangu? Akasema: Hakika mimi nilikuwa nikiswali. Mtume akasema: Hivi Mwenyezi Mungu hajasema: “Enyi mlioamini mwitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume anapokuiteni kwa yale yatakayokupeni uzima.”<sup>36</sup>

Akasema: Kisha Mtume wa Mwenyezi Mungu akasema: ‘Nitakufundisha Sura tukufu mno ndani ya Qur'ani. Alipokuwa kama kasahau nikamwambia: ‘Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu uliyoyasema.’ Mtume akasema: Al-Hamdu lillahi Rabil-alamina ndio saba zisomwazo mara kwa

---

35. *Tafsirut-Tabari*: 14/38

36. *Al-Anfal*: 24

## Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara

mara na Qur'ani tukufu ambayo nimepewa.”<sup>37</sup>

Ad-Darqutni na Al-Bayhaqiy wametoa toka kwa Abi Huraira kuwa Mtume alikuwa akianza kwa “Bismillahi Rahmani Rahim” pindi asomapo, ilihali akiwaswalisha watu. Abi Huraira akasema: ‘Ni Aya ndani ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu, isomeni mtakapo kusoma ufunguo wa Kitabu (Al-Hamdu) hakika yenyewe ni Aya ya saba.”<sup>38</sup>

Ad-Darqutni na Al-Bayhaqiy ndani ya As-Sunan wametoa kwa njia sahihi toka kwa Abdu Khayri amesema: “Ali (R.a) aliulizwa kuhusu saba zisomwazo mara kwa mara, akasema: "Ni Al-Hamdu lillahi Rabil-alamina.” Akaambiwa: Hakika yenyewe ina Aya sita!’ Akasema: “Bismillahi Rahmani Rahim” ni Aya.”<sup>39</sup>

Ibnu Al-Ambariyu ametoa ndani ya *Al-Maswahifu* toka kwa Ummu Salama amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu alisoma: Bismillahi Rahmani Rahim\*

(Kila sifa njema ni za Mwenyezi Mungu, Mola wa viume)\*

(Mwingi wa rehema mwenye kurehemu)\*

(Mwenye kumiliki siku ya malipoi)\*

(Wewe tu tunakuabudu, na kwako tu tunataka msaada)\*

(Tuongoze njia iliyo nyooka)\*

(Njia ya wale uliowaneemesha, siyo ya waliokasirikiwa, wala ya waliopotea)\*

Akasema: “Ndio saba ewe Ummu Salama.”<sup>40</sup>

---

37. *Tafsiri Tabariy*: 14/41

38. *As-Sunnanil-Kubra*: 2/47. *Sunanud-Darqutniy*: 1/305

39. *Sunanid-Darqutniy*: 1/311. *Sunannil-Kubra*: 2/45

40. *Ad-Durul-Manthur*: 1/12

## **Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara**

---

# **AL-HAMDU, UFUNGUO WA KITABU NI AYA SABA IWAPO PAMOJA NA BISMILLAHI**

Hakika Al-Hamdu ni Aya saba iwapo tu tutasema kuwa Bismillahi ni sehemu ya Al-Hamdu, na kwa ajili hiyo unaona Misahafu maarufu inahesabu kuwa Bismillahi ni Aya ya Surat Al-Fatihah japokuwa inaacha kuihesabu kuwa ni Aya katika Sura nyingine, kwa maana hiyo idadi ya Aya saba inakuwa kwa namna ifuatayo:

Bismillahi Rahmani Rahim (1)\*

Kila sifa njema ni za Mwenyezi Mungu, Mola wa viume (2)\*

Mwingi wa rehema mwenye kurehemu (3)\*

Mwenye kumiliki siku ya malipoi (4)\*

Wewe tu tunakuabudu, na kwako tu tunataka msaada (5)\*

Tuongoze njia iliyo nyooka (6)\*

Njia ya wale uliowaneemesha, siyo ya waliokasirikiwa, wala ya waliopotea (7)

Unaona kila Aya ni sentensi kamili. Ama yule asiyejalia Bismillahi kuwa ni miongoni mwa Aya saba yeye amejalia (Njia ya wale uliowaneemesha) kuwa ni Aya na (Siyo ya wale waliokasirikiwa, wala ya waliopotea) kuwa ni Aya nyingine. Maana yake kajalia Kuibadilishwa ni Aya na mbadala ni Aya nyingine, na jambo hili halikubaliani na fasaha sahihi.

## **Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara**

Pia yupo aliyejaribu kuifanya (Wewe tu tunakuabudu) Aya na (Na kwako tu tunataka msaada) Aya nyingine. Hakika amepita njia ngumu ya kutisha, hakika sentensi hizi mbili ni kipande kimoja cha fedha safi ambacho kinaeleza tauhidi katika ibada na kuomba msaada, hivyo nini maana ya kuzitenganisha.

Hizi ni baadhi tu ya riwaya za masuni zinazoonyesha kuwa Bismillahi ni sehemu ya Surati Al-Fatihah, huku pia zikionyesha mambo mengine mawili:

Utakaloliona mbele kuwa Mtume (s.a.w.) yeye na maswahaba zake walikuwa wakidhihirisha Bismillahi.

2. Zinaonyesha pia kuwa Bismillahi ni sehemu ya kila Sura

Isipokuwa kutokana na mpangilio wa uchambuzi wa mada husika tume-tenganisha kati ya riwaya zinazoonyesha kudhihirisha Bismillahi wakati wa kusoma Al-Fatihah na zile zinazozungumzia Bismillahi. Pia tukatenganisha zile zinazoonyesha kuwa Bismillahi ni sehemu ya kila Sura.

## **Riwaya za Maimam wa Ahlul-Bayt**

Ama riwaya zilizipokewa toka kwa Maimam wa Ahlul-Bayt zinasimulia wala hamna matatizo. Na hapa tutataja baadhi tu ya zile zilizopokewa toka kwao (a.s.):

Sheikh ametoa ndani ya *Tahdhibu* toka kwa Muhammad bin Muslim amesema: “Nilimuuliza Abiu Abdillah (a.s.) kuhusu saba zisomwazo mara kwa mara na Qur'ani tukufu, je, ni Surati Al-Fatihah? Akasema: Ndio. Nikasema: Je, Bismillahi Rahmani Rahim ni katika hizo saba? Akasema:

## Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara

Ndio, na ndio bora yao.”<sup>41</sup>

Sheikh ametoa ndani ya *Tahdhibu* toka kwa Abdallah bin Yahya Al-Kahiliy toka kwa Abu Abdillah (a.s.) toka kwa baba yake amesema: Bismillahi Rahmani Rahim ndio iliyo karibu mno na jina tukufu la Mwenyezi Mungu kuliko ukaribu wa mboni ya jicho kwenye weupe wake.”<sup>42</sup>

Al-Kulayniy ametoa toka kwa Muawiya bin Ammari amesema: Nilimwambia Abi Abdallah (a.s.), nikisimama kwa ajili ya Swala nisome Bismillahi Rahmani Rahim ndani ya ufunguo wa Kitabu (Al-Hamdu)? Akasema: Ndio.”<sup>43</sup>

As-Saduq ametoa ndani ya *Uyunil-Akh'bari* toka kwa Al-Hasani bin Ali Al-Askari (a.s.) amesema: “Kiongozi wa waumini (a.s.) aliambiwa tupe habari kuhusu Bismillahi Rahmani Rahim, Je ni sehemu ya ufunguo wa Kitabu (Al-Hamdu)? Akasema: Ndio, Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa akiisoma na kuihesabu kuwa ni Aya na akisema: Ufunguo wa Kitabu (Al-Hamdu) ndio saba zisomwazo mara kwa mara.”<sup>44</sup>

Na kuna riwaya nyingine zaidi ya hizo toka kwa Maimam wa Ahlul-Bayt kuhusu usehemu wa Bismillahi katika Surat Al-Fatihah.

Na kinachounga mkono hilo ni riwaya mashuhuri toka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu aliposema: “Kila jambo la muhimu lisiloanzwa kwa Bismillahi halitimii, na kila jambo la muhimu lisiloanzwa kwa Bismillahi halina matunda au haliendelei.”<sup>45</sup>

---

41. *At-Tahdhib*: 2/289, namba 1157

42. *At-Tahdhib*: 2/289 namba 1159

43. *Al-Kafiy*: 3/312, hadithi ya 1

44. *Uyunul-Akh'bari Ridha*.

45. *At-Tafsir al-Kabir* ya Razi: 1/198

## **Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara**

Maalum ni kuwa Qur'ani ndio ufunuo bora kati ya ufunuo alioufunua Mwenyezi Mungu kwa manabii wake na mitume wake, na kila Sura ya Qur'ani ina umuhimu na utukufu ambao Mwenyezi Mungu aliwaomba wanadamu walete mfano wake wakashindwa kuleta mfano wake. Je, inawezekana Qur'ani isitimie?

Ametakasika Mwenyezi Mungu, na ufunuo wake wenye hekima umetakasika, na Sura zake ziko mbali mno na uongo huo.

Swala ndio kufaulu na ndio amali bora kama inavyonadiwa juu ya minara na mimbari, jambo ambalo analijua mtu wa zamani hadi wa kisasa, haku-na kitu kinacholingana na Swala baada ya imani ya kumuamini Mwenyezi Mungu, Vitabu Vyake, Mitume Wake na Siku ya Mwisho. Je, inasihhi Mwenyezi Mungu alete sheria isiyo na faida au isiyo na maendeleo?!

Hakika hakuna jasiri yoyote muovu wala mwema anayeweza kusema hilo. Lakini Maimam wema Malik, Al-Awazaiyi na Abi Hanifa (r.a.) wameghafilika na matokeo hayo ya lazima.

Na kila Mujtahid anayetoa hukumu toka kwenye vyanzo vyake vya kishe-ria atasamehewa na atalipwa sawa apatie au akosee.<sup>46</sup>

## **Bismillahi na ulazima wa kudhihirishwa**

Kutokana na uchambuzi uliyopita imethibiti kuwa Bismillahi ni sehemu ya ufunuo wa Kitabu (Al-Hamdu) na ni sehemu yake muhimu, hivyo Sura hiyo haitimii isipokuwa kwa kuisoma.

---

46. *Masailu Fiqhiyatu*: 28-29

## Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara

Ama kuhusu kuidhirisha, hukumu yake ni sawa na hukumu ya vifungu vingine vya Sura hiyo, hivyo iwapo Swala ni miongoni mwa Swala za kudhirisha basi ni lazima kuidhirisha ilimradi tu haijapatikana dalili inayoruhusu kuisoma kwa kimya kimya.

Zaidi ya hapo ni kuwa kuna riwaya nyingi zimekuja zikionyesha ulazima wa kuidhirisha, na hilo tunaweza kulipata toka ndani ya riwaya zifuatazo:

Al-Hakim ametoa toka kwa Abi Huraira amesema: “Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa akidhirisha Bismillahi Rahmani Rahim.”<sup>47</sup>

Al-Hakim ametoa toka kwa Anas bin Malik amesema: “Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu akidhirisha Bismillahi Rahmani Rahim. Akasema: Wapokezi wa hadithi hii wa kwanza mpaka wa mwisho wao ni waaminifu. Na Adh-Dhahabiyu akathibitisha hilo ndani ya *Talkhisi* yake.”<sup>48</sup>

Al-Hakim ametoa ndani ya *Mustadrak* yake toka kwa Muhammad bin Abi Al-Siriyu Al-Asqalani amesema: Niliswali nyuma ya Al-Mu'tamaru bin Sulaymani siku nyingi, Swala za Asubuhi na Magharibi kwa idadi isiyohesabika na alikuwa akidhirisha Bismillahi Rahmani Rahim kabla ya ufunguo wa Kitabu (Al-Hamdu) na baada yake.”

Na nilimsikia Al-Mu'tamaru akisema: “Nimeapa sintoacha kufuata Swala ya baba yangu, na baba yangu alisema: Nimeapa sitoacha kufuata Swala ya Anas bin Malik, na Anas bin Malik alisema: Nimeapa sintoacha kufuata Swala ya Mtume wa Mwenyezi Mungu.”

Wapokezi wa hadithi hii wote ni waaminifu kuanzia wa mwanzo mpaka wa mwisho. Na Adh-Dhahabiy amethibitisha hilo ndani ya *Talkhis* yake.”<sup>49</sup>

---

47. *Al-Mustadrak*: 1/232

48. *Al-Mustadrak*: 1/232

49. *Al-Mustadrak*: 1/232

## **Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara**

Al-Hakim ametoa toka kwa Humaidu Al-Tawilu toka kwa Anas amesema: Niliswali nyuma ya Mtume na nyuma ya Abi Bakr na nyuma ya Umar na nyuma ya Uthman na nyuma ya Ali na wote walikuwa wakidhihirisha kwa kusoma Bismillahi Rahmani Rahim.”

Kisha akasema: Katika mlango mwingine zimebakia riwaya nyingine toka kwa Uthman na Ali, Talha bin Ubaydullah, Jabiri bin Abdullah, Abdallah bin Umar, Al-Hukmu bin Umayri At-Thamaliy, Nu'mani bin Bashir, Samratu bin Jundub na Aisha binti Abi Bakr, zote zimetolewa ninazo mlango mzima, nimeziacha ili kufupisha hivyo nikaishia kutoa zile tu zinazohusiana na mlango huu. Pia katika mlango huo wametajwa maswahaba na waliokuja baada ya maswahaba waliodhihirisha Bismillahi Rahmani Rahim.”<sup>50</sup>

Kwa kuwa maneno ya mwisho ambayo yanadai kuwa Maimam wote walikuwa wakidhihirisha Bismillahi ndani ya Swala yanapingana na madhehebu ya Imam wa Adh-Dhahabiy hasira zikampanda na kudai kuwa kunasibisha udhihirishaji wa kisomo cha Bismillahi kwa watu hawa ni uongo mtupu.

Kisha akaapa kuwa madai yake ndio kweli, ilihali Mtume anasema: Ushahidi ni kwa yule anayedai, na kiapo cha yamini ni kwa yule anayekanusha.

Hivyo anayedai kuwa ni uongo ni lazima alete ushahidi si kiapo, na kama atashindwa basi kila atakayekuwa anaona Hadithi inapingana na matakwa yake na madhehebu yake aliyokulia atataka aape kuonyesha uongo wa hadithi hiyo.

---

50. *Al-Mustadrak*: 1/232



### **Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara**

5. Riwaya aliyoipokea Shafi'i ndani ya *Musnadi* yake kuwa Muawiya alikwenda Madina akaswali hapo Madina, na wala hakusoma Bismillahi Rahmani Rahim, hivyo Muhajirina na Ansvari wakamkosoa kwa kusema: Ewe Muawiya, umetuibia Swala, iko wapi Bismillahi Rahmani Rahim?!

Kisha Shafi'i akaongeza kwa kusema: “Laiti kama kudhihirisha Bismillahi kusingekuwa ni jambo lililokubalika kwa maswahaba wote Muhajirina na Ansvari basi wasingeweza kudhihirisha ukosoaji wao kwake kwa sababu ya kuacha Bismillahi.”

- 6- Na Al-Hakim ameitoa kwa namna nyingine akasema: Hakika Anas bin Malik amesema: Muawiya aliswalisha Swala moja huko Madina akawa amedhihirisha kisomo, akasoma ndani ya kisomo hicho Bismillahi Rahmani Rahim kwa ajili ya Mama wa Qur'ani (Al-Hamdu) na wala hakusoma Bismillahi Rahmani Rahim kwa ajili ya Sura nyingine ambayo ilifuata baada ya Al-Hamdu mpaka alipomaliza kusoma Sura hiyo. Alipomaliza Muhajirina na Ansvari waliosikia hilo walimuita toka kila sehemu: Umeiba Swala au umesahau?!

Aliposwali baada ya tukio hilo alisoma Bismillahi Rahmani Rahim kwa ajili ya Sura iliyokuja baada ya Mama wa Qur'ani, na akawa anatoa takbira anapokwenda kusujudu.

Al-Hakim amesema: “Hadithi hii ni sahihi kwa mujibu wa sharti za Muslim, kwani Abdul-Majid bin Abdul-Aziz ni hoja kwake, yeye na wapokezi wengine ambao uadilifu wao umekubalika. Na Adh-Dhahabiy amethibitisha hilo ndani ya *Talkhis* yake.

- 7- Razi ndani ya tafsiri yake amesema: “Hakika Al-Bayhaqiy amepokea kudhihirishwa kwa Bismillahi Rahmani Rahim ndani ya Sunani yake toka kwa Umar bin Al-Khattabi, na Ibnu Abbas, na Ibnu Umar na Ibnu Zuberi.”

## Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara

Kisha Razi akasema: “Hili ndilo tamko lake: Ama kuwa Ali alikuwa akidhihirisha Bismillahi hilo limethibiti kwa uwingi na atakayemfuata Ali katika dini yake basi ameongoka.” Akasema: Na dalili juu ya hilo ni kauli ya Mtume: ‘Ewe Mwenyezi Mungu izungushe haki pamoja na Ali popote atakapozunguka.’<sup>51</sup>

8. Al-Bazaru na Ad-Darqutniy na Al-Bayhaqiy ndani ya *Shaabul-Imani* wametoa kwa njia ya Abi Tufayl amesema: “Nilimsikia Ali bin Abi Talib na Ammari wakisema: ‘Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alikuwa akidhihirisha Bismillahi Rahmani Rahim katika Surati Al-Fatihah ndani ya Swala za faradhi.’<sup>52</sup>

9. Ad-Darqutniy ametoa toka kwa Aisha kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa akidhihirisha Bismillahi Rahmani Rahim.<sup>53</sup>

10 Ad-Darqutniy ametoa toka kwa Nu'man bin Bashir amesema: “Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: Aliniswalisha Jibril kwenye Al-Kaaba akadhihirisha Bismillahi Rahmani Rahim.”<sup>54</sup>

11 Ad-Darqutniy ametoa toka kwa Ali bin Abi Talib (a.s.) amesema: “Mtume alikuwa akidhihirisha Bismillahi Rahmani Rahim ndani ya Sura zote mbili.”<sup>55</sup>

12 Ad-Darqutniy na Al-Hakim na Al-Bayhaqiy wametoa toka kwa Abi Huraira kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa akidhihirisha Bismillahi Rahmani Rahim ndani ya Swala. Na Al-Bayhaqiy akaongeza: “Watu wakaacha kufanya hivyo.”<sup>56</sup>

---

51. *Tafsirul-Kabir*: 1/204

52. *Sunnanud-Darqutniy*: 1/302. *Shaabul-Imani*: 2/436 hadithi ya 2322, mlango wa kutukuza Qur'ani. *Ad-Durul-Manthur*: 1/21 na 22

53. *Ad-Durul-Manthur*: 1/23

54. *Sunnanud-Darqutniy*: 1/309. *Ad-Durul-Manthur*: 1/22

55. *Sunnanud-Darqutniy*: 1/302. *Ad-Durul-Manthur*: 1/22

56. *Mustadrakul-Hakim*: 1/208. *As-Sunnanil-Kubra*: 2/48.

*Sunnanud-Darqutniy*: 1/306

### **Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara**

13. Ad-Darqutniy ametoa toka kwa Abdallah bin Umar amesema: “Niliswali nyuma ya Mtume na Abu Bakr na Umar na walikuwa wakidhihirisha Bismillahi Rahmani Rahim.”<sup>57</sup>
14. Ath-Tha'labiy ametoa toka kwa Ali bin Zaid bin Jadiani kuwa kina Abdallah watatu walikuwa wakianza Swala kwa kusoma Bismillahi Rahmani Rahim wakiidhihirisha: Yaani ni Abdallah bin Abbas, Abdallah bin Umar na Abdallah bin Zuberi<sup>58</sup>
15. Al-Bayhaqiy ametoa toka kwa Az-Zahriy amesema: “Miongoni mwa Sunna za Swala ni usome Bismillahi Rahmani Rahim, na wa kwanza kuisoma Bismillahi Rahmani Rahim kwa kimya kimya ni Said bin Al-Aas huko Madina na alikuwa ni mtu mwenye haya sana.”<sup>59</sup>
16. Ad-Darqutniy ametoa toka kwa Abi Huraira amesema: “Mtume wa Mwenyezi Mungu alisema: Jibril alinifundisha Swala akasimama na akatutolea takbira kisha akasoma: Bismillahi Rahmani Rahim akidhihirisha ndani ya kila rakaa.”<sup>60</sup>
17. Ad-Darqutniy ametoa toka kwa Al-Hakamu bin Umayr - alipigana vita vya Badri - amesema: “Niliswali nyuma ya Mtume akadhihirisha Bismillahi ndani ya Swala na Swala za usiku na Swala ya Al-fajiri na Swala ya Ijumaa.”<sup>61</sup>

Razi ametoa hoja ya ulazima wa kudhihirisha Bismillahi ndani ya Swala za kudhihirisha kwa kutumia tuliyoyasema mwanzo wa uchambuzi huu, kuwa hukumu ya sehemu ya Sura ndio hukumu ya Sura nzima, na wala haisihi kubagua kati ya Sura nzima na sehemu yake isipokuwa kwa dalili yakini-fu. Razi amelitaja hilo kwa tamko lifuatalo:

57. Sunnanud-Darqutniy: 1/305. Durul-manthuri: 1/22

58. Ad-Durul-Manthur: 1/21

59. Ad-Durul-Manthur: 1/21

60. Sunnanud-Darqutniy: 1/305. Ad-Durul-Manthur: 1/20 na 21.

61. Sunnanud-Darqutniy: 1/308. Ad-Durul-Manthur: 1/22 na 23.

## **Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara**

Tumeshatoa dalili kuwa Bismillahi ni Aya ndani ya Surat Al-Fatihah, likithibiti hili basi tunasema: Hali halisi imeonyesha kuwa Sura moja ima yote nzima iwe inasomwa kimya kimya au kwa kudhihirisha.

Ama kudai kuwa baadhi yake isomwe kwa kimya na baadhi nyingine kwa kudhihirisha jambo hili halipo katika Sura zote. Ikithibiti hili basi inakuwa kudhihirisha Bismillahi ni sheria katika kisomo cha kudhihirisha.<sup>62</sup>

## **Maimam wa Ahlul-Bayt na kudhihirisha Bismillahi**

Kuna riwaya nyingi toka kwa Maimam wa Ahlul-Bayt zinazothibitisha kudhihirisha Bismillahi. Mwenendo wa Imam Ali (a.s.) na Maimam waliokuja baada yake ulikuwa ni kuidhihirisha. Hapa tutagusia baadhi ya riwaya hizo toka kwao:

Sheikh Abi Al-Fatuhu Razi ametoa ndani ya *Tafsir* yake toka kwa Ridha toka kwa baba yake toka kwa As-Sadiq (a.s.) amesema: “Kizazi cha Muhammad wote wamejumuika kwenye kudhihirisha “Bismillahi Rahmani Rahim.”<sup>63</sup>

Ali bin Ibrahim ametoa ndani ya *Tafsir* yake toka kwa njia yake toka kwa Ibnu Udhayna amesema: “Abi Abdalla (a.s.) amesema: “Bismillahi Rahmani Rahim” ndio yenye haki sana ya kudhihirishwa, na yenyewe ndio Aya ambayo Mwenyezi Mungu amesema: “Na unapomtaja Mola wako katika Qur'ani peke yake, basi wao hugeuza migongo yao kwa chuki”<sup>64, 65</sup>

As-Saduq ametoa kwa njia yake toka kwa Al-Aamashi toka kwa Jafar bin

---

62. *Tafsir Al-Kabir*: 1/204

63. *Raudhul-Janani*: 1/50. *Al-Mustadrak* ya Shekhe Nuuriyu: 4/189 namba 4456

64. *Al-Israi*: 46

65. *Tafsiri Al-Qumiy*: 1/28

## Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara

Muhammad (a.s.) kuwa alisema: “Kudhihirisha Bismillahi Rahmani Rahim ndani ya Swala ni wajibu.”<sup>66</sup>

As-Saduq ametoa kwa njia yake toka kwa Al-Fadh'lu bin Shadhani kuwa ndani ya ujumbe aliomuandikia Ridha (a.s.) Ma'amuni katika kubainisha uhalisi wa Uislamu, imeandikwa: ‘Na kudhihirisha Bismillahi Rahmani Rahim ndani ya Swala zote ni Sunna.’<sup>67</sup>

Imepokewa toka kwa Ridha (a.s.) kuwa alikuwa akidhihirisha Bismillahi Rahmani Rahim ndani ya Swala zake zote za usiku na mchana.<sup>68</sup>

Al-Kulayniy ametoa toka kwa Swafuani Al-Jammali amesema: “Niliswali nyuma ya Abi Abdallah siku nyingi, ikiwa Swala si ya kudhihirisha alikuwa akidhihirisha Bismillahi Rahmani Rahim, na alikuwa akiidhihirisha kwenye Sura mbili.”<sup>69</sup>

Al-Ayashi ametoa toka kwa Khalid Al-Mukhtari amesema: “Nilimsikia Jafar bin Muhammad akisema: ‘Wana nini! wameizushia uongo makusudi Aya tukufu mno ndani ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu wakadai eti ni bidaa wanapoidhihirisha, nayo ni Bismillahi Rahmani Rahim.’”<sup>70</sup>

Al-Kulayniy ametoa toka kwa Yahya bin Abi Imrani Al-Hamdaniy amesema: “Nilimuandikia Abi Jafar Al-Jawad (a.s.): Nimekutolea fidia, unase-maje kuhusu mtu anayeanza kwa Bismillahi Rahmani Rahim ndani ya Swala yake asomapo Mama wa Kitabu (Sura ya Al-Hamdu), anapofika kwenye Sura nyingine isiyokuwa mama wa Kitabu (Al-Hamdu) anaiacha Bismillahi?” Al-Abasiyu akesema: “Kufanya hivyo si vibaya.”

66. *Al-Khisali*: 2/604, mlango wa mia moja na zaidi namba 9

67. *Uyunul-Akh'bar Ridhaa*: 2/122, mlango 35

68. *Uyunul-Akh'bar Ridhaa*: 2/181, mlango 44 namba 5

69. *Al-Kafiy*: 3/315, hadithi ya 20

70. *Tafsiril-Ayashi*: 1/21 Hadithi ya 16.

## **Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara**

Al-Jawadi akaandika kwa hati yake: "Anatakiwa kuirudia mara mbili japo anakarahishwa (yaani Al-Abasiyu).<sup>71</sup>

Natarajia kuwa riwaya zilizotajwa zinatoshwa kabisa kwa yule mtafuta haki na msaka ukweli.

## **Hoja za mwenye kudai kuwa Bismillahi si sehemu ya Al-Fatihah au haidhihirishwi**

Hakika ukweli umedhihirika kwa mdhihiriko wake wa wazi, na ukaonekana kupitia dalili za wazi kuwa Bismillahi ni sehemu ya Al-Fatihah na kuwa hudhihirishwa kwa wajibu ndani ya Swala za kudhihirisha.

Na kuna riwaya za ajabu zinazoonyesha kuwa ima Mtume aliiacha kabisa au hakuidhihirisha, lakini madhumuni ya baadhi ya riwaya hizo ni dalili ya wazi juu ya uongo wa riwaya husika na kuwa riwaya hizo zilipandikizwa. Hapa tutazitaja moja baada ya nyingine.

1. Muslim ametoa toka kwa Shaabatu amesema: "Nilimsikia Qatadatu akisimulia toka kwa Ibnu Abbas kuwa alisema: 'Niliswali na Mtume wa Mwenyezi Mungu na Abu Bakar na Umar na Uthman sikumsikia hata mmoja kati yao akisoma Bismillahi Rahmani Rahim.'"
2. Ameitoa tena kwa njia nyingine toka kwa Anas bin Malik kuwa alisema: "Niliswali nyuma ya Mtume wa Mwenyezi Mungu na Abu Bakr na Umar na Uthman na walikuwa wakianza Swala kwa "Al-Hamdulillahi Rabil-Aalamina" hawasomi "Bismillahi Rahmani Rahim" mwanzo wa kisomo wala mwisho wake.<sup>72</sup>

**Anajibiwa kuwa:** Riwaya hizi zinapingana na ile aliyoitoe Al-Hakim toka

<sup>71</sup>. Al-Kafiy: 3/313, hadithi ya 2

<sup>72</sup>. Sahih Muslim: 2/12 mlango wa hoja ya mwenye kusema kuwa Bismillahi haidhihirishwi.

### **Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara**

kwa Anas bin Malik kuwa alisema: “Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu akidhihirisha Bismillahi Rahmani Rahim.”<sup>73</sup>

Hivyo kutokana na mgongano huu haiwezekani kutegemea hizo riwaya mbili. Razi ametosheleza katika kujibu hadithi hizo mbili ambazo ndio tegemezi la wenye kusema aliacha au hakudhihirisha, Razi amesema: Sheikh Abi Hamid Al-Asfarayaniy amesema: Katika mlango huu kuna riwaya sita zimepokea toka kwa Anas. Ama wafuasi wa Hanafi wenyewe wamepokea riwaya tatu toka kwake:

Mojawapo ni kauli yake: ‘Niliswali nyuma ya Mtume na nyuma ya Abu Bakr na Umar na Uthman na walikuwa wakianza Swala kwa Al-Hamdulillahi Rabil-Aalamina.

Ya pili ni kauli yake: “Hakika wao walikuwa hawasomi Bismillahi Rahmani Rahim.”

Ya tatu ni kauli yake: “Sikumsikia hata mmoja kati yao akisema Bismillahi Rahmani Rahim.”

Hivyo hizi riwaya tatu zinaipa nguvu kauli ya wafuasi wa Hanafi, na tatu nyingine zinatengua kauli zao:

Mojawapo: Ni ile tuliyoitaja kuwa Anas amepokea kuwa Muawiya alipoacha Bismillahi Rahmani Rahim, Muhajirina na Answari walimkosoa, na tumebainisha kuwa jambo hili linaonyesha kuwa kudhihirisha maneno haya ( Bismillahi) ni kama jambo lililopokea kwa wingi kati yao.

Ya pili ni: Abi Qalabatu amepokea toka kwa Anas kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu na Abu Bakr na Umar walikuwa wakidhihirisha Bismillahi Rahmani Rahim.

Ya tatu ni: Aliulizwa kuhusu kudhihirisha au kuisoma kwa siri Bismillahi Rahmani Rahim akasema: “Suala hili silijui.”

---

<sup>73</sup>. Angalia namba 4 Bismillahi na ulazima wa kudhihiriswa. Hadithi ya 2 na 4

### **Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara**

Hivyo inathibiti kuwa riwaya toka kwa Anas zinazohusu suala hili zina mchanganyiko na utata mkubwa sana, hivyo zimebakia zikipingana na imewajibika kurejea kwenye dalili nyingine.

Shafi'i amesema: "Huenda makusudio ya kauli ya Anas kuwa Mtume alikuwa akianza Swala kwa Al-Hamdulillahi Rabil-Aalamina, yaani alikuwa akiitanguliza Sura hii katika kisomo kabla ya nyingine. Hivyo makusudio ya tamko lake: Al-Hamdulillahi Rabil-Aalamina ni Sura nzima, hivyo akawa amelifanya tamko hili kuwa jina la Sura hii."

Pia kuna tuhuma nyingine nayo ni kuwa Ali alikuwa amezidisha kudhihirisha Bismillahi, hivyo dola ilipofika mikononi mwa Bani Ummaya walizidisha kuzuia kuidhihirisha, ikiwa ni kujitahidi kubatilisha athari za Ali (a.s.). Hivyo huenda Anas aliwaogopa na kutokana na sababu hii kauli zake zikatatanisha.

Na hata kama tukishakia kitu chochote kile lakini hakika sisi hatushakii kuwa, hakika kuchukua kauli ya Ali (a.s.) ni bora katika hali yoyote ile ya kuwepo mgongano kati ya kauli ya Anas na kauli ya Ali bin Abi Talib ambayo alidumu nayo umri wake wote.

Hivyo hili ni jibu tosha katika suala hili.

3. Ibnu Abi Shaybatu na Tirmidhiy na An-Nasa'iy na Ibnu Maja na Al-Bayhaqiy wote wametoa toka kwa Abdallah bin Magh'falu amesema: "Baba alinisikia nikisoma: Bismillahi Rahmani Rahim; akasema: 'Ewe mwanangu mpendwa, umezua? Niliswali nyuma ya Mtume wa Mwenyezi Mungu na Abu Bakr na Umar na Uthman sikumsikia hata mmoja kati yao akidhihirisha Bismillahi Rahmani Rahim.'"<sup>74</sup>

---

74. *Sunani Al-Bayhaqiy: 2/522. Durul-Manthuri: 1/29*



## **Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara**

Razi amejibu hadithi hii kwa kusema: Hakika jawabu ni kwa vigezo vifu-atavyo:

Kwanza: Hakika mpokezi wa habari zenu ni Anas na Ibnu Maghfalu, na mpokezi wa habari zetu ni Ali bin Abi Talib, Ibnu Abbas, Ibnu Umar na Abi Huraira na hawa walikuwa ndio wenye elimu nyingi na ukaribu mno na Mtume kuliko Anas na Ibnu Maghfalu.

Pili: Ni maalumu kuwa hali halisi ni kuwa Mtume alikuwa akiwatanguliza wakubwa kabla ya wadogo, wasomi kabla ya wasio wasomi, wenye sharafu kabla ya mabedui, na hakuna shaka kuwa Ali na Ibnu Abbas na Ibnu Umar walikuwa na hali ya juu kielimu, kisharafu na kidaraja kuliko Anas na Ibnu Maghfalu.

Na nina dhana ya juu kabisa kuwa Ali na Ibnu Abbas na Ibnu Umar walikuwa wakisimama karibu zaidi na Mtume na Anas na Ibnu Maghfalu walikuwa wakisimama mbali na Mtume.

Na pia Ali (a.s.) hakuwa anazidisha kudhihirisha kwa ajili ya kutekeleza kauli ya Mwenyezi Mungu: “Wala usiiseme swala yako kwa sauti kubwa, wala usiiseme kwa sauti ndogo, bali shika njia baina ya hizo”.<sup>75</sup>

Pia mwanadamu anapoanza kusoma huanza kwa sauti ya chini kisha muda uendavyo ndivyo aongezavyo sauti. Hivyo sababu hizi ni vigezo dhahiri vilivyowafanya Ali na Ibnu Abbas na Ibnu Umar na Abi Huraira waisikie Bismillahi toka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, na Anas na Ibnu Maghfalu wasiisikie.

**TATU:** Huenda makusudio ya kutokudhihirisha katika hadithi ya Ibnu Maghfalu ni kutokuzidisha kuinua sauti, kama alivyosema Mwenyezi Mungu: “Wala usiiseme Swala yako kwa sauti kubwa, wala usiiseme kwa sauti ndogo.”

---

75. **Al-Israa:** 110

### **Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara**

Nne: Hakika dalili za kiakili zinaafikiana na sisi, na kitendo cha Ali bin Abi Talib kipo pamoja na sisi, na atakaemfanya Ali Imam wa dini yake basi kwa hakika ameshikamana na kishikio imara ndani ya dini yake na nafsi yake.

4- Riwaya iliyopokewa toka kwa Abi Huraira kuwa Mtume alisema: 'Mwenyezi Mungu amesema: Nimeigawa Swala nusu mbili kati yangu na mja wangu, hivyo mja wangu anaposema: (Kila sifa njema ni za Mwenyezi Mungu, Mola wa viumbe)\* Mwenyezi Mungu husema: Mja wangu amenihimidi.

Akisema: (Mwingi wa rehema mwenye kurehemu)\* Mwenyezi Mungu husema: Mja wangu amenisifu.

Akisema: (Mwenye kumiliki siku ya malipo)\* Mwenyezi Mungu husema: Mja wangu amenitukuza.

Akisema: (Wewe tu tunakuabudu, na kwako tu tunataka msaada)\* Mwenyezi Mungu husema: Hili ni kati yangu na mja wangu.

Hoja ya habari hii ni kwa kutumia vigezo viwili:

Kwanza: Mtume (s.a.w.w.) hajaitaja Bismillahi, na laiti kama Bismillahi ingekuwa ni Aya ndani ya Surat Al-Fatihah basi angeitaja.

Pili: Mwenyezi Mungu amesema: Nimeifanya Swala nusu mbili kati yangu na mja wangu, na makusudio ya Swala hapa ni Al-Fatihah. Nusu hii inapatikana iwapo tu tutasema kuwa Bismillahi si Aya ndani ya Surat Al-Fatihah, kwa sababu Al-Fatihah ni Aya saba.

Hivyo inawajibika Mwenyezi Mungu awe na Aya tatu na nusu, nazo ni kuanzia kauli: ( Kila sifa njema ni za Mwenyezi Mungu) mpaka (Wewe tu tunakuabudu).

Na mja awe na Aya tatu na nusu nazo ni kuanzia (Wewe tu tunakuabudu na

## **Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara**

kwako tu tunataka msaada) mpaka mwisho wa Sura.

Ama tukijalia kuwa Bismillahi Rahmani Rahim ni Aya ndani ya Surat Al-Fatihah basi Mwenyezi Mungu atakuwa na Aya nne na nusu na mja atakuwa na Aya mbili<sup>76</sup> na nusu, hivyo ule unusu uliotajwa utabatilika.<sup>77</sup>

Anajibiwa kuwa; Kwanza: Habari hii inapingana na habari iliyovushwa toka kwa Ibnu Abbas inayosema: “Nimegawa Swala kati yangu na mja wangu, hivyo mja wangu akisema: (Bismillahi Rahmani Rahim) Mwenyezi Mungu husema: Mja wangu ameniita....mpaka mwisho wa hadithi.

Riwaya hii imejumuisha Bismillahi, na ndani ya riwaya hii iliyovushwa toka kwa Ibnu Abbas hamna neno nusu mbili, na mgawanyo haulazimishi kuwepo usawa wa idadi.

Razi amesema: Hakika tamko “nusu” kama linavyoweza kumaanisha nusu katika idadi ya Aya ndivyo linavyoweza kumaanisha nusu kimaana. Mtume amesema: “Faradhi ni nusu ya elimu”, ameziita nusu kwa kuwa uchambuzi kuhusu hali za maiti na umauti na uhai ni vigawanyo viwili.

Pili: Hakika Abi Huraira amepokea kuhusu kudhihirisha Bismillahi Rahmani Rahim toka kwa Mtume, na yeye mwenyewe alikuwa akiidhihirisha huku akisema: Hakika Swala yangu ndio ifananayo sana na Swala ya Mtume. Hadithi yake kuhusu hilo imeshatangulia.<sup>78</sup>

5-Imepokewa toka kwa Aisha kuwa Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akianza Swala kwa kutoa takbira na kusoma Al-Hamdulillahi Rabil-Aalamina, na hii inaonyesha kuwa Bismillahi si Aya ndani ya Surat Al-Fatihah.

Anajibiwa kuwa: Hakika Aisha amefanya Al-Hamdulillahi Rabil-

76. Chanzo cha maelezo haya kimeandikwa hivyo lakini sahihi ni tatu

77. Al-Tafsiri Al-Kabir: 1/201

78. Angalia hadithi ya kumi na mbili.

## **Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara**

Aalamina kuwa jina la Sura hii. Hiyo ni kama inavyosemwa: Fulani amesoma (Kila sifa njema ni za Mwenyezi Mungu ambaye kaumba mbingu) na makusudio ya hapo ni kuwa kasoma Sura hii. Na ndio hivyo hivyo hapa.

Nasema: Kuna Sura nyingi zinaitwa kutumia Aya zake za mwanzo, hivyo husemwa: Fulani amesoma Sura (Sema: Yeye Mwenyezi Mungu ni mmoja) .

Au amesoma Sura (Vinamsabihi Mwenyezi Mungu vile vilivyomo mbinguni). Na mfano wa hizo.

Hivyo maana ya hadithi inakuwa ni kuwa alikuwa akianza Swala kwa kutoa takbira na kusoma Sura ambayo mwanzo ni “Bismillahi Rahmani Rahim..... mpaka mwisho.”<sup>79</sup>

## **Zinazopingwa na historia sahihi**

Tabaraniy ametoa kwa njia ya Said bin Jubairi toka kwa Ibnu Abbas kuwa alisema: Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa asomapo Bismillahi Rahmani Rahim, mushrikina hutetemeka na kusema: Muhammad anataja Mungu wa Al-Yamama, na Musaylamatu alikuwa akijiita Rahmani, hivyo iliposhuka Aya hii Mtume akaamrisha isidhihirishwe.<sup>80</sup>

Hii ndio ile ile aliyoitoa Ibnu Daud toka kwa Said bin Jubairi amesema: “Mtume alikuwa akidhihirisha Bismillahi Rahmani Rahim, na watu wa Makka walikuwa wakimuita Musaylamatu Rahmani, hivyo wakasema: ‘Hakika Muhammad analingania Mungu wa Al-Yamama, ndipo Mtume akaamrisha ifichwe, na kuanzia hapo haikudhihirishwa mpaka alipoku-fa.”<sup>81</sup>

79. Al-Tafsiri Al-Kabir: 1/202

80. At-Tabaraniy ndani ya Al-Awsatu: 5/89. Durul-Manthur: 1/29

81. Ad-Durul-Manthur: 1/29

## Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara

Lakini historia inapinga riwaya hii katika hali yoyote ile hata kama njia yake ni sahihi au imevushwa mvusho salama, kwa sababu jambo la Musaylama halikuvuma isipokuwa ndani ya mwaka wa kumi Hijiria, ni umbali uliyoje kati ya alipo yeye na kuhama kwa Mtume na mwanzo wa utume!

Tabariy na wengine wamepokea kuwa Musaylama alikwenda na ujumbe kwa Mtume akiwa na jamaa zake na akawa amesilimu, aliporudi mji wake wa makazi akadai unabii, akazungukwa na jamaa zake kwa ajili ya chuki, mpaka imepokewa kuwa kuna kipindi mmoja kati ya wafuasi wake alimuuliza Musaylama akisema: “Ni nani anaekujia?”

Musaylama akajibu: “Rahmani.”

Muulizaji akasema: “Katika hali ya nuru au katika hali ya giza?”

Akajibu: “Katika hali ya giza.”

Muulizaji akasema: Nashuhudia kuwa hakika wewe ni muongo, na hakika Muhammad ni mkweli, lakini muongo wa Rabiata anapendwa sana kwetu kuliko mkweli wa Mudhari.<sup>82</sup>

Sheikh wetu, Maarifa, amesema: “Waarabu walikuwa wanajua “Rahmani” na kuwa ndie Mola wa ulimwengu (Na husema: Angelipenda Rahmani tusingewaabudu).<sup>83</sup>

(Wakasema: Nyinyi si chochote ila ni watu kama sisi, wala Rahmani hakuteremsha chochote).<sup>84</sup>

Mwenyezi Mungu amezungumza nao kwa sifa hii zaidi ya sehemu hamsi-ni. Waliweza vipi kukanusha sifa hii kwa Mwenyezi Mungu na kudaiwa

---

82. *Tarekhu Tabari: 2/508.*

83. **Zukhrufu:** 20

84. **Yasini:** 15

## Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara

kuwa imeazimwa toka kwenye sifa ya mtu wa Al-Yamama?!

Ama kauli ya Mwenyezi Mungu: (Na wanapoambiwa: Msujudieni Rahmani, husema: Ni nani Rahmani? Je, tumsujudie unayetuamuru? Na inawazidishia chuki).<sup>85</sup> Kukanusha kwao si dalili ya kutomjua, kwani hakika kauli yao: (Ni nani Rahmani?) ni sawa na kauli ya Firauni: (Ni nani Mola wa ulimwengu?). Ni kudhihaki nafasi ya msemaji anaelingania ibada ya Mwenyezi Mungu na kuwa yeye ni Mungu mmoja asiye na mshirika.

7- Ibnu Shaybatu ametoa toka kwa Ibnu Abbas kuwa amesema: "Kudhihirisha Bismillahi Rahmani Rahim ni kisomo cha mabedui."<sup>86</sup>

Sema kweli mbele ya Mwenyezi Mungu, je, hivi Imam Ali ambaye alikuwa maarufu kwa kudhihirisha Bismillahi katika Swala zake zote alikuwa ni bedui?

Na je Imam Shafi'iy na wenzake waliopokea toka kwake au waliojifunza kwake, ambao walikuwa wakiidhihirisha katika Swala za kudhihirisha je na wao walikuwa ni mabedui?! (Mmekuwaje, mnahukumu namna gani?)

8 - Mfano wa hiyo ni ile aliyoitoa Ibnu Abi Shayba toka kwa Ibrahim An-Nakhaiyu amesema: Imamu kudhihirisha Bismillahi Rahmani Rahim ni bidaa.<sup>87</sup>

Maimam ambao Ibrahim amechukua fiq'hi kutoka kwao walikuwa wakidhihirisha Bismillahi, hivi je, alichukua fiq'hi toka kwa wapandikizi wa mambo ndani ya dini?

Hayo yote yanathibitisha kuwa kuegemeza kauli hizi kwa maimamu wa hadithi na fiq'hi ni uongo uliyozushwa.

Mpaka hapa umetimia uchambuzi kuhusu mambo mawili yafuatayo:

---

85. **Al-Furqani: 60**

86. *Musnafu Ibnu Abi Shaybatu: 1/441. Durul-Manthur:1/29*

87. *Al-Musanafu: 1/448. Durul-Manthur: 1/29-30*

## **Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara**

1. Bismillahi ni sehemu ya Al-Fatihah (Al-Hamdu)
2. Bismillahi hudhihirishwa ndani ya Swala za kudhihirisha.

## **Bismillahi ni sehemu ya mwanzo wa kila Sura**

Uchambuzi uliopita umekuwezesha kujua kuwa bila shaka Bismillahi ni sehemu ya Surat Al-Fatihah, na kuwa ni lazima idhihirishwe ndani ya Swala za kudhihirishwa.

Uchambuzi umebaki kuhusu jambo la tatu nalo ni kuwa Bismillahi ni sehemu ya mwanzo wa kila Sura isipokuwa Surat Tauba. Dalili juu ya hilo ni:

**Kwanza:** Maswahaba wote, kisha wote waliokuja baada ya maswahaba na waliokuja baada ya wale waliokuja baada ya maswahaba, kisha kila walio-pita katika umma huu, toka walipoandika Qur'ani mpaka leo, wote wameafikiana kivitendo juu ya kuandika Bismillahi mwanzo wa kila Sura ila Surati Tauba.

Wameiandika kama walivyoandika Aya nyingine bila ya kuweka alama inayotenganisha, huku wao wote wakiungana mkono kuwa wasiandike chochote kisicho Qur'ani isipokuwa kwa kukiwekea alama tetenganishi ili ndani ya Qur'ani msichanganyikane na kitu kisicho Qur'ani.

Hivi huoni jinsi walivyoitenganisha Qur'ani na majina ya Sura zake, na alama za vifungu vyake ( juzuu), makundi yake, robo zake, tano zake na kumi zake, hivyo wakaweka hayo nje ya Sura kwa namna ambayo itajulikana kuwa mambo hayo yako nje ya Qur'ani, hiyo yote ni kuihifadhi Qur'ani na kuichukulia tahadhari.

Natarajia unajua kuwa ni mara chache sana umma wote kuafikiana juu ya

### **Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara**

jambo kama walivyoafikiana juu ya hilo. Hivyo jambo hili lenyewe tu ni dalili tosha kuwa Bismillahi Rahmani Rahim ni Aya kamili yenye kujitegemea mwanzo wa kila Sura, waliotangulia hadi waliofuata wameiandika mwanzo wa Sura.<sup>88</sup>

**Pili:** Al-Hakim ametoa toka kwa Ibnu Abbas kuwa ilikuwa Mtume (s.a.w.w.) akijiwa na Jibril na akasoma Bismillahi Rahmani Rahim ndipo hujua kuwa ni Sura mpya. Hadithi hii ina njia sahihi lakini mashekhe wawili hawajaitoa.<sup>89</sup>

**Tatu:** Al-Hakim ametoa toka kwa Ibnu Abbas (R.a.) kuwa amesema: “Mtume alikuwa hajui mwisho wa Sura mpaka inapoteremka Bismillahi Rahmani Rahim.”

Al-Hakim amesema: “Hii ni hadithi sahihi kwa mujibu wa sharti za mashekhe wawili na hawajaitoa. Al-Dhahabiyu amekiri usahihi wake ndani ya muhtasari wa *Al-Mustadrak*.”<sup>90</sup>

**Nne:** Al-Hakim ametoa toka kwa Ibnu Abbas amesema: “Waislamu walikuwa hawajui kuisha kwa Sura mpaka inapoteremshwa Bismillahi Rahmani Rahim, ikiteremshwa Bismillahi Rahmani Rahim ndipo wanapojua kuwa Sura imekwisha.”<sup>91</sup>

**Tano:** Ibnu Dharisu amepokea toka kwa Ibnu Abbas amesema: “Bismillahi Rahmani Rahim ni Aya.”<sup>92</sup>

---

88. *Masailul-Fiqihiyati*: 28

89. *Al-Mustadrak*: 1/231

90. *Al-Mustadrak*: 1/231

91. *Al-Mustadrak*: 1/232.

92. *Ad-Durul-Manthur*: 1/20



### **Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara**

**Sita:** Al-Wahidiyu ametoa toka kwa Abdallah bin Umar amesema: “Bismillahi Rahmani Rahim iliteremshwa ndani ya kila Sura.”<sup>93</sup>

**Saba:** Tabaraniy ametoa ndani ya Al-Awsatu na Darqutniy na Al-Bayhaqiy toka kwa Nafi'u kuwa Ibnu Umar alikuwa anapoanza Swala husoma Bismillahi Rahmani Rahim katika Mama wa Kitabu (Al-Hamdu) na katika Sura ambayo inafuatia, na kusema kuwa alisikia hilo toka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu.<sup>94</sup>

(Na limetimia neno la Mola wako kwa kweli na uadilifu, hakuna awezaye kuyabadilisha maneno yake, na yeye ndiye mwenye kusikia, mwenye kujua).<sup>95</sup>

Imetafsiriwa na:

Hemedi Lubumba Selemani.

Simu **0773-017178.**

**0715-017178.**

**0754-017178.**

---

93. *Ad-Durul-Manthur*:1/20

94. *Ad-Durul-Manthur*:1/22

95. *Al-an'ami*:115

**Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara**

---

**ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA  
AL-ITRAH FOUNDATION:**

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka kumi na sita
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu

### **Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara**

---

27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
36. Amateka
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
39. Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Nyuma yaho naje kuyoboka
41. Amavu n'amavuko by'ubushiya
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Kusujudu juu ya udongo
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Maulid
47. Bismillahi ni sehemu ya Qur'ani
48. Malumbano baina ya Sunni na Shia

## Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara

---

### BACK COVER

#### BISIMILLAH NI SEHEMU YA QUR'AN

Sheria ya Kiislamu ni ya kipekee kwa kuwa inahusika na kila jambo huku ikiweka utatuji wa matatizo yote yanayompata mwanadamu katika sekta zote za maisha yake, hivyo Mwenyezi Mungu akasema:

**"Leo nimewakamilishieni dini yenu na kuwatimizieni neema Yangu na nimewapendeleeni Uislamu uwe dini yenu." (5:3).**

Isipokuwa kuna masuala madogo madogo ambayo wanazuoni wa sheria wamehitilafiana kwa sababu ya kutofautiana kwao kuhusu riwaya ambazo zimenasibishwa kwa Mtume. Jambo ambalo limesababisha kutofautiana kuhusu masuala madogo madogo ya sheria.

Kwa kuwa ukweli hutokana na utafiti basi hakika katika mtiririko wa masomo haya mwandishi amejaribu kuliweka swala hili juu ya meza ya utafiti, kwani huenda ikawa ndio njia ya kuunganisha mtazamo na kusogeza hatua katika uwanja huu.

Kwani tofauti iliyopo si katika asili na misingi ya dini hata isababishwe kuwa na uadui na chuki, bali tofauti iliyopo ni kuhusu riwaya zilizonasibishwa na Mtume, nalo ni jambo dogo ukilinganisha na mambo mengi ambayo tunaafikiana kati ya madhehebu za Kiislamu. Na mwongozo wetu katika njia hii ni kauli ya Mwenyezi Mungu:

**"Na shikamaneni katika kamba ya Mwenyezi Mungu nyote wala msifarakiane. Na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yenu, mlipokuwa maadui na akaziunganisha nyoyo zenu, hivyo kwa neema Zake mkawa ndugu." (3:103)**

## **Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara**

---

Kimetolewa na kuchapishwa na:

**Al-Itrah Foundation**

P.O. Box 19701,

Dar es Salaam, Tanzania

Simu: +255 22 2110640

Simu/Fax: +255 22 2127555

Email:alitrh@raha.com